04

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR

# TOLEO LA TAKWIMU ZA AJALI NA MAKOSA YA BARABARANI ZANZIBAR, APRILI, MWAKA 2024

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

## Utangulizi

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ajali na makosa ya barabarani. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (11).


## Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera, na watoa maamuzi.

## Ajali za Barabarani

Jumla ya ajali 18 zimeripotiwa mwezi wa Aprili, 2024. Wilaya ya Kaskazini ‘A’ na Kaskazini ‘B’ zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni nne (4) kwa kila wilaya sawa na asilimia 22.2 ikilinganishwa na wilaya nyengine.


**Kielelezo 1.1: Idadi ya Ajali za Barabarani Kwa Wilaya, Aprili 2024**




Idadi ya ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Aprili, 2024 zimeongezeka kwa asilimia 28.6 kufikia ajali 18 kwa mwezi wa Aprili 2024 kutoka ajali 14 mwezi wa Machi 2024

Kwa mwezi wa Aprili 2024, Wilaya ya Kaskazini ‘A’ na Kaskazini ‘B’ zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ( ajali nne (4)) kwa kila wilaya na wilaya ya Kati iliripotiwa kuwa na ajali zaidi( ajali tatu (3)) kwa mwezi wa Machi 2024


**Kielelezo 1.2: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani kwa Mwezi wa Machi 2023 na Aprili 2024**



Idadi ya Ajali za barabarani kwa mwaka zimeongezeka kwa asilimia 28.6 na kufikia ajali 18 kwa mwezi wa Aprili 2024 kutoka ajali 15 kwa mwezi wa Aprili 2023.


Kwa mwezi wa Aprili 2024, wilaya ya Kaskazini ‘A’ na Kaskazini ‘B’ imeripotiwa kuwa na ajali nne (4) kwa kila wilaya na Aprili 2023 wilaya ya Magharibi “A” ilikuwa na ajali zaidi, nne (4).

**Kielelezo 1.3: Mlinganisho wa Ajali za Barabarani Kwa Mwezi wa Aprili 2023 na Aprili 2024**





Jumla ya waathirika 38 wameripotiwa mwezi wa Aprili, 2024, ambapo waathirika 27 walikuwa wanaume na waathirika 11 alikuwa wanawake. Wilaya ya Kaskazini ‘A’ imeripotiwa kuwa na waathirika wengi ambao ni 13 sawa na asilimia 34.2 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika wa Ajali za Barabarani, Aprili 2024**





Waathirika waliofariki kwa mwezi Aprili 2024 wameongezeka kwa asilimia 62.5 kufikia waathirika 13 waliofariki kwa mwezi wa Aprili 2024 kutoka waathirika nane (8) waliofariki kwa mwezi wa Machi 2024.

**Kielelezo 1.5: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Machi 2024 na Aprili 2024**




Waathirika waliojeruhiwa kwa mwezi uliopita wameongezeka kwa asilimia 31.6 na kufikia waathirika 25 waliojeruhiwa mwezi wa Aprili, 2024 kutoka waathirika 19 waliojeruhiwa kwa mwezi wa Machi, 2024.

**Kielelezo 1.6: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Machi 2024 na April 2024**





Waathirika waliofariki kwa mwezi wa Aprili 2024 wameongezeka kwa asilimia 8.3 hadi kufikia waathirika 13 waliofariki mwezi wa Marchi 2024 kutoka waathirika 12 waliofariki kwa mwezi wa Aprili 2023.

**Kielelezo 1.7: Mlinganisho wa Waathirika Waliofariki kwa Mwezi wa Aprili 2023 na Aprili 2024**





Waathirika waliojeruhiwa kwa mwezi wa Aprili 2024 wameongezeka na kufikia waathirika 25 kutoka waathirika 13 waliojeruhiwa mwezi wa Aprili 2023.

**Kielelezo 1.8: Mlinganisho wa Waathirika Waliojeruhiwa kwa Mwezi wa Aprili 2023 na Aprili 2024**




Mwezi wa Aprili, 2024 waathirika wengi ( waathirika 22) walikuwa abiria kati ya waathirika 38. Miongoni mwa waathirika wa ajali za barabarani (waliojeruhiwa na waliofariki), abiria walikuwa 22, wapanda baiskeli na pikipiki 10, waenda kwa miguu watano (5) na dereva alikuwa mmoja (1).

**Kielelezo 1.9: Idadi na Aina ya Waathirika wa Ajali za barabarani, Aprili 2024**





Kwa mwezi wa Aprili 2024, ajali zaidi zilitokea muda wa saa 03:01 - 06:00 mchana na saa 12:01jioni - 03:00 usiku ambapo zimeripotiwa ajali tano (5) kwa kila saa.

**Kielelezo 1.10: Idadi ya Ajali na Muda Uliotokea, Aprili 2024**




Jumla ya ajali 18 zilizoripotiwa mwezi wa Aprili, 2024, ajali 13 zimesababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi na ajali tano (5) zimesababishwa na uzembe wa dereva. Mkoa wa Kaskazini Unguja unaongoza kwa kuwa na ajali zilizosababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi (ajali 6).

**Kielelezo 1.11: Chanzo cha Ajali za Barabarani kwa Mkoa, Aprili 2024.**




## Makosa ya Barabarani

Jumla ya makosa 1,826 yameripotiwa mwezi wa Aprili 2024, ambapo makosa 1,821 yameripotiwa kwa wanaume na makosa matano (5) yameripotiwa kwa wanawake.

Wilaya ya Magharibi “A” ina idadi kubwa ya makosa ya barabarani (makosa 422) sawa na asilimia 23.1 kati ya makosa yote yaliyoripotiwa. Wilaya ya Wete ina idadi ndogo ya makosa ya barabarani yaliyoripotiwa ambayo ni makosa 37 (asilimia 2.0) kati ya makosa yote yaliyoripotiwa.


**Kielelezo 2.0: Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Wilaya, Aprili 2024**




Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwezi wa Aprili 2024 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani **(makosa 697)** yakifuatia Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo **(makosa 346)** na Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia **(makosa 237).**

Orodha ya makosa haya matatu (3) ya barabarani kati ya yote kumi (10) yaliyoripotiwa yamechangia asilimia 70.1


**Kielelezo 2.1: Idadi na Aina ya Makosa ya Barabarani, Aprili 2024**



Idadi ya makosa kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 40.6 na kufikia makosa 1,826 kwa mwezi wa Aprili 2024 kutoka makosa 3,073 mwezi wa Machi 2024 .

Wilaya ya Magharibi "A" imeongoza kwa mwezi wa Aprili 2024 (Makosa 422) na mwezi wa Machi 2024 (makosa 759) kuwa na idadi kubwa ya makosa.


**Kielelezo 2.2: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Mwezi wa Machi 2024 na Aprili 2024**




Idadi ya makosa kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 50.4 na kufikia makosa 1,826 kwa mwezi wa Aprili 2024 kutoka makosa 3,064 kwa mwezi wa Aprili 2023.

Wilaya ya Magharibi "A" imeongoza kwa mwezi wa Aprili 2024 (makosa 422) na mwezi wa Aprili, 2023 wilaya ya Kati iliongoza kwa makosa ya barabarani (makosa 779).

**Kielelezo 2.3: Mlinganisho wa Idadi ya Makosa ya Barabarani kwa Mwezi wa Aprili 2023 na Aprili 2024**



## HITIMISHO

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (11). Lengo la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar.

Jumla ya ajali 18 zimeripotiwa mwezi wa Aprili, 2024. Wilaya ya Kaskazini 'A' na Kaskazini 'B' zimeripotiwa kuwa na ajali zaidi ambazo ni nne (4) kwa kila wilaya sawa na asilimia 22.2 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

Mlinganisho wa Idadi ya ajali za barabarani zilizotokea kwa mwezi Aprili, 2024 zimeongezeka kwa asilimia 28.6 kufikia ajali 18 kwa mwezi wa Aprili 2024 kutoka ajali 14 mwezi wa Machi 2024.

Jumla ya makosa 1,826 yameripotiwa mwezi wa Aprili 2024, ambapo makosa 1,821 yameripotiwa kwa wanaume na makosa matano (5) yameripotiwa kwa wanawake.

Kosa kuu lililoripotiwa kwa mwezi wa Aprili 2024 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (**makosa 697**) sawa na asilimia 38.2 ya makosa yote yaliyoripotiwa.

## Kiambatanisho:

**Jadweli 3.0: Idadi na Asilimia ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; April2024**

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Waliokufa | | | | Waliojeruhiwa | | | | Jumla | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Nambari | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia |
| Kaskazini 'A' | 4 | 22.2 | 2 | 0 | 2 | 15.4 | 4 | 7 | 11 | 44.0 | 6 | 7 | 13 | 34.2 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 22.2 | 1 | 0 | 1 | 7.7 | 4 | 0 | 4 | 16.0 | 5 | 0 | 5 | 13.2 |
| Kati | 1 | 5.6 | 1 | 0 | 1 | 7.7 | 2 | 0 | 2 | 8.0 | 3 | 0 | 3 | 7.9 |
| Kusini | 1 | 5.6 | 1 | 0 | 1 | 7.7 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 1 | 0 | 1 | 2.6 |
| Mjini | 1 | 5.6 | 1 | 0 | 1 | 7.7 | 1 | 0 | 1 | 4.0 | 2 | 0 | 2 | 5.3 |
| Magharibi 'A' | 3 | 16.7 | 1 | 3 | 4 | 30.8 | 2 | 1 | 3 | 12.0 | 3 | 4 | 7 | 18.4 |
| Magharibi 'B' | 2 | 11.1 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 2 | 0 | 2 | 8.0 | 2 | 0 | 2 | 5.3 |
| Wete | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| Micheweni | 1 | 5.6 | 1 | 0 | 1 | 7.7 | 2 | 0 | 2 | 8.0 | 3 | 0 | 3 | 7.9 |
| Chake chake | 1 | 5.6 | 2 | 0 | 2 | 15.4 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 2 | 0 | 2 | 5.3 |
| Mkoani | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 | 0 | 0 | 0 | 0.0 |
| **Zanzibar** | **18** | **100** | **10** | **3** | **13** | **100** | **17** | **8** | **25** | **100** | **27** | **11** | **38** | **100** |

## Jadweli 3.1: Idadi ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Aprili 2024

| Wilaya | Idadi ya Ajali | Dereva | | | | | | Abiria | | | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | | | Waendao kwa Miguu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | |
| | | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| Kaskazini 'A' | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 7 | 10 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 |
| Magharibi 'A' | 3 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 2 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **18** | **0** | **1** | **1** | **0** | **0** | 0 | **1** | **2** | **3** | **11** | **8** | **19** | **7** | **0** | **7** | **3** | **0** | **3** | **2** | **0** | **2** | **3** | **0** | **3** |

## Jadweli 3.2: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya Mwezi wa Machi 2024 na Aprili 2024

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Waathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Mac-24 | Apr-24 | Mac-24 | Apr-24 | Mac-24 | Apr-24 | Mac-24 | Apr-24 | Mac-24 | Apr-24 | Mac-24 | Apr-24 | Mac-24 | Apr-24 | Mac-24 | Apr-24 | Mac-24 | Apr-24 | Mac-24 | Apr-24 | Mac-24 | Apr-24 |
| Kaskazini 'A' | 2 | 4 | 1 | 11 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 2 | 4 | 3 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 3 | 1 | 6 | 2 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 1 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Mjini | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 |
| Magharibi 'A' | 2 | 3 | 3 | 3 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 3 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi 'B' | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 1 | 2 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 1 | 1 | 2 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **14** | **18** | **19** | **25** | **8** | **13** | **2** | **0** | **0** | **1** | **9** | **19** | **2** | **3** | **6** | **3** | **5** | **7** | **2** | **3** | **1** | **2** |

### Jadweli 3.3: Mlinganisho wa Idadi ya Ajali Barabarani baina ya Mwezi Aprili 2023 na Aprili 2024

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Walioathirika | | | | Dereva | | | | Abiria | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | Waendao kwa Miguu | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | | Waliojeruhiwa | | Waliokufa | |
| | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 |
| Kaskazini 'A' | 3 | 4 | 4 | 11 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 0 | 4 | 1 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 4 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 2 | 1 | 1 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Kusini | 2 | 1 | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Mjini | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 4 | 3 | 1 | 3 | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 3 | 0 | 2 | 1 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi 'B' | 1 | 2 | 2 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Wete | 1 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 1 | 1 | 0 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Chake Chake | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **15** | **18** | **13** | **25** | **12** | **13** | **0** | **0** | **0** | **1** | **2** | **19** | **1** | **3** | **10** | **3** | **8** | **7** | **1** | **3** | **3** | **2** |

**Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa Kwa Wilaya na Jinsi, Aprili 2024**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | | Uendeshaji Hatari | | | Ubovu wa Vipando | | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 7 | 42 | 0 | 42 | 62 | 0 | 62 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 13 | 0 | 13 | 6 | 0 | 6 | 11 | 0 | 11 | 9 | 0 | 9 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 17 | 0 | 17 | 69 | 0 | 69 | 38 | 0 | 38 | 37 | 0 | 37 | 43 | 0 | 43 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 18 | 0 | 18 | 12 | 0 | 12 | 30 | 0 | 30 | 17 | 0 | 17 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 21 | 0 | 21 | 19 | 0 | 19 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 0 | 11 | 27 | 0 | 27 | 94 | 0 | 94 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 0 | 20 | 18 | 0 | 18 | 54 | 0 | 54 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 9 | 0 | 9 | 5 | 0 | 5 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 0 | 9 | 11 | 0 | 11 | 18 | 0 | 18 |
| Chake chake | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 16 | 3 | 19 | 14 | 0 | 14 | 23 | 0 | 23 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 16 | 2 | 18 | 19 | 0 | 19 | 11 | 0 | 11 |
| **Zanzibar** | **1** | **0** | **1** | **32** | **0** | **32** | **93** | **0** | **93** | **141** | **5** | **146** | **237** | **-** | **237** | **346** | **0** | **346** |

## Inaendelea… Jadweli 3.4: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa kwa Wilaya na Jinsi, Aprili 2024

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva kwa gari za abiria | | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 22 | 0 | 22 | 71 | 0 | 71 | 0 | 0 | 0 | 204 | 0 | 204 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 44 | 0 | 44 |
| Kati | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 38 | 0 | 38 | 48 | 0 | 48 | 3 | 0 | 3 | 296 | 0 | 296 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 16 | 0 | 16 | 3 | 0 | 3 | 26 | 0 | 26 | 124 | 0 | 124 |
| Mjini | 37 | 0 | 37 | 0 | 0 | 0 | 19 | 0 | 19 | 113 | 0 | 113 | 0 | 0 | 0 | 209 | 0 | 209 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 31 | 0 | 31 | 259 | 0 | 259 | 0 | 0 | 0 | 422 | 0 | 422 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 13 | 0 | 13 | 165 | 0 | 165 | 0 | 0 | 0 | 270 | 0 | 270 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 8 | 0 | 8 | 14 | 0 | 14 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 37 | 0 | 37 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 7 | 0 | 7 | 0 | 0 | 0 | 50 | 0 | 50 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 17 | 0 | 17 | 26 | 0 | 26 | 0 | 0 | 0 | 97 | 3 | 100 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 10 | 0 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 0 | 12 | 68 | 2 | 70 |
| **Zanzibar** | **40** | **0** | **40** | **18** | **0** | **18** | **175** | **0** | **175** | **697** | **0** | **697** | **41** | **0** | **41** | **1,821** | **5** | **1,826** |

**Jadweli 3.5: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Aprili, 2023 na Aprili, 2024**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji Hatari | | Ubovu wa Vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 25 | 0 | 44 | 0 | 1 | 7 | 66 | 42 | 95 | 62 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 12 | 13 | 28 | 6 | 1 | 11 | 67 | 9 | 98 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 20 | 17 | 93 | 69 | 3 | 38 | 39 | 37 | 107 | 43 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 18 | 11 | 12 | 11 | 30 | 20 | 17 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 26 | 0 | 29 | 21 | 19 | 19 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 42 | 11 | 104 | 27 | 29 | 94 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 34 | 20 | 68 | 18 | 24 | 54 |
| Wete | 0 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 12 | 1 | 61 | 9 | 12 | 5 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 9 | 11 | 11 | 2 | 18 |
| Chake chake | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 23 | 19 | 14 | 14 | 29 | 23 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 18 | 14 | 19 | 30 | 11 |
| **Zanzibar** | **1** | **1** | **60** | **32** | **166** | **93** | **174** | **146** | **484** | **237** | **465** | **346** |

Inaendelea… Jadweli 3.5: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Aprili, 2023 na Aprili, 2024

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 | Aprili 2023 | Aprili 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 55 | 22 | 356 | 71 | 0 | 0 | 642 | 204 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 25 | 0 | 268 | 5 | 1 | 0 | 500 | 44 |
| Kati | 27 | 3 | 0 | 0 | 155 | 38 | 335 | 48 | 0 | 3 | 779 | 296 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 80 | 16 | 105 | 3 | 0 | 26 | 227 | 124 |
| Mjini | 0 | 37 | 0 | 0 | 13 | 19 | 182 | 113 | 0 | 0 | 269 | 209 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 99 | 31 | 215 | 259 | 0 | 0 | 489 | 422 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 133 | 13 | 194 | 165 | 0 | 0 | 453 | 270 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 8 | 2 | 14 | 28 | 0 | 0 | 0 | 119 | 37 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 9 | 7 | 0 | 0 | 23 | 50 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 0 | 10 | 17 | 21 | 26 | 0 | 0 | 97 | 99 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 10 | 9 | 0 | 8 | 0 | 0 | 12 | 81 | 70 |
| **Zanzibar** | **27** | **40** | **-** | **18** | **581** | **175** | **1,721** | **697** | **1** | **41** | **3,680** | **1,825** |

**Jadweli 3.6: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Machi 2024 na Aprili 2024**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | Uendeshaji Hatari | | Ubovu wa Vipando | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia | | Kuzidisha idadi ya abiriana mizigo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 3 | 0 | 10 | 0 | 0 | 7 | 25 | 42 | 57 | 62 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 5 | 13 | 8 | 6 | 0 | 11 | 24 | 9 | 77 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 27 | 17 | 102 | 69 | 85 | 38 | 93 | 37 | 117 | 43 |
| Kusini | 0 | 0 | 2 | 2 | 21 | 18 | 48 | 12 | 27 | 30 | 35 | 17 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 17 | 0 | 29 | 21 | 102 | 19 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 14 | 11 | 97 | 27 | 180 | 94 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 11 | 20 | 32 | 18 | 68 | 54 |
| Wete | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 | 0 | 3 | 1 | 28 | 9 | 14 | 5 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 4 | 9 | 18 | 11 | 12 | 18 |
| Chake chake | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 9 | 19 | 80 | 14 | 0 | 23 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 | 18 | 17 | 19 | 34 | 11 |
| **Zanzibar** | **0** | **1** | **42** | **32** | **147** | **93** | **211** | **146** | **470** | **237** | **696** | **346** |


**Inaendelea… Jadweli 3.6: Idadi ya Makosa Barabarani, baina ya Mwezi wa Machi 2024 na Aprili 2024**

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani ya mmiliki wa gari | | Kughushi nyaraka za serikali kwa gari za abiria | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa Utingo na dereva kwa gari za abiria | | Kutofuata miongozo na kanuni za usalama barabarani | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawili kwenye Chombo za Maringi Mawili | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 | Machi 2024 | Aprili 2024 |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 15 | 22 | 113 | 71 | 3 | 0 | 226 | 204 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 30 | 0 | 167 | 5 | 0 | 0 | 311 | 44 |
| Kati | 7 | 3 | 12 | 0 | 0 | 38 | 0 | 48 | 108 | 3 | 551 | 296 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 30 | 16 | 20 | 3 | 28 | 26 | 211 | 124 |
| Mjini | 0 | 37 | 0 | 0 | 34 | 19 | 126 | 113 | 0 | 0 | 308 | 209 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 71 | 0 | 0 | 31 | 397 | 259 | 0 | 0 | 759 | 422 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 43 | 13 | 182 | 165 | 0 | 0 | 336 | 270 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 8 | 6 | 14 | 29 | 0 | 0 | 0 | 88 | 37 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 9 | 5 | 6 | 7 | 0 | 0 | 51 | 50 |
| Chake chake | 0 | 0 | 23 | 0 | 0 | 17 | 17 | 26 | 0 | 0 | 130 | 100 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 10 | 18 | 0 | 13 | 0 | 0 | 12 | 102 | 70 |
| **Zanzibar** | **7** | **40** | **106** | **18** | **185** | **175** | **1,070** | **697** | **139** | **41** | **3,073** | **1,826** |


**Jadweli 3.7 Tozo zilizolipwa Mahakamani Kwa Wilaya na Idadi ya kesi, Aprili 2024**

| Wilaya | Idadi ya kesi | Tozo(Shilingi) |
|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 242 | 4,568,000 |
| Kaskazini 'B' | 319 | 7,150,600 |
| Kati | 235 | 4,988,000 |
| Kusini | 182 | 2,359,000 |
| Mjini | 421 | 12,540,000 |
| Magharibi 'A' | 325 | 8,800,000 |
| Magharibi 'B' | 156 | 5,397,000 |
| Wete | 37 | 990,000 |
| Micheweni | 50 | 1,161,500 |
| Chake chake | 97 | 1,150,500 |
| Mkoani | 73 | 2,345,500 |
| **Zanzibar** | **2,137** | **51,450,100** |

**Kielelezo1: Ajali za Barabarani za Barabarani Zilizoripoti kwa Wilaya, Aprili 2024**



**Kielelezo 2:Vifo na Majeruhi Wanaotokana na Ajali za Barabarani kwa Wilaya, Machi 2024**



## Zingatia Maelezo

Ajali ya barabarani inahusu ajali yeyote inayohusisha angalau gari moja barabarani, inayotokea barabarani kwa mzunguko wa umma na angalau mtu mmoja amekufa au amejeruhiwa. Kutokana na Sheria ya Adhabu nambari.6/2004 kuondoa Amri ya Adhabu, sura ya 13 ya sheria ya Zanzibar (Penal Act no. 6/2004 Act to repeal the Penal Decree, chapter 13 of the law of Zanzibar).

Kifo imefafanua iwapo kama watu wamepata ajali na kufa papo hapo au ndani ya mwaka mmoja na siku moja (366) baada ya ajali.

Watu waliojeruhiwa na waathirika kwa ajali waliopatwa na mshtuko wanaohitaji matibabu ya Hospitali au bila hospitali.

Njia kimsingi ina maana ya usafiri. Hio humpa binadamu kufikia maeneo tofauti. Watu wengi hutumia njia tofauti za usafiri. Baadhi yao hutumia gari, baiskeli na kwa miguu.

Kosa ni uhalifu ambao huvunja sheria fulani na kuwepo adhabu maalum. Ajali za barabarani husababishwa na makosa mbalimbali ya binadamu. Makosa mengi ambayo yanaonekana kuwa ni madogo lakini athari yake inakuwa kubwa. Matokeo yake watu hupata ulemavu au kufa.

**KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**


**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua, 2321,
Simu: +255242231869,
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com,
Nukushi: 024223136,
MMP, Zanzibar